**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Ndugu Wanahabari;**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imepewa Mamlaka ya Kikatiba na Kisheria katika kusimamia masuala yote ya Haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Ibara 129 (1), 130(1),(c),(f) na (g) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na vifungu vya 6 (1) (c) na (g), 15 (1) (a) na 28 (1) (a), (b) na (f) vya Sheria ya THBUB Sura 391, vimeipa Tume mamlaka ya kuchunguza jambo lolote linaloashiria au kuthibitisha uvunjwaji wa haki za binadamu au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini.

**Ndugu Wanahabari;**

Kwa kuzingatia mamlaka hiyo THBUB imekuwa ikipokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kutoka kwa wananchi au kwa THBUB kuanzisha uchunguzi yenyewe baada ya kupata taarifa ya matukio yanayoashiria uvunjwaji wa haki za binadamu kupitia vyombo vya habari.

Kwa ujumla THBUB imeongeza kasi ya ushughulikiaji wa malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kutokana na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya uchunguzi. Kwa mfano kwa mwaka 2022/2023 THBUB ilikuwa ikishughulikia jumla ya

malalamiko 1524 ambapo ilihitimisha jumla ya malalamiko 789 na kufanya malalamiko yaliyoendelea kuanzia 1 Julai, 2023 kuwa ni 885.

Aidha, katika kipindi cha kuanzia tarehe 01 Julai 2023 hadi 30 Mei, 2024, THBUB ilipokea malalamiko mapya 135 na kufanya malalamiko yaliyokuwa yanashughulikiwa mwaka huo kuwa ilikuwa inashughulikia jumla ya malalamiko 1020 ambapo katika kipindi husika THBUB ilifanikiwa kukamilisha na kuhitimisha uchunguzi wa malalamiko 236 na hivyo uchunguzi wa malalamiko 784 unaendelea. Katika malalamiko hayo, 302 yanahusu maslahi na stahili za watumishi mfano mafao ya kustaafu, kutowasilishwa michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na malimbikizo ya mishahara. Masuala hayo huhitaji mawasiliano na mamlaka zinazohusika ili kuyapatia ufumbuzi tofauti na malalamiko ambayo huilazimu THBUB kufanya uchunguzi maalum kwa kufika eneo la tukio kwa ajili ya kukusanya ushahidi na vielelezo ili kupata ukweli kuhusu malalamiko au tuhuma zilizotolewa.

Katika malalamiko hayo, malalamiko ishirini na mbili yaliyoilazimu THBUB kufanya uchunguzi maalum. Chunguzi hizo zilihusu masuala ya ardhi, uharibifu wa mazingira, tuhuma za vitendo vya ukatili katika vizuizi na matumizi mabaya ya madaraka.

Malalamiko na chunguzi ambazo zimekamilika ni kama ifuatavyo:-

i. Uchunguzi kuhusu Wananchi kutwaliwa maeneo yao na uongozi wa Kijiji cha Mbabala B ekari zipatazo 37, kata ya mbabala, Jiji la Dodoma, Mkoa wa Dodoma; Oktoba 2023. Uchunguzi huu ulifanyika kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na wananchi dhidi ya Afisa Mtendaji wa Mtaa wa Mwongozo na Afisa Mtendaji wa Kata ya Mbabala wakidai kuwa maeneo yao yamechukuliwa na kuendelezwa na viongozi hao bila kulipwa fidia.

ii. Uchunguzi wa mgogoro wa ardhi na madai ya uvunjifu wa haki za binadamu kati ya wananchi wa vijiji vya Sikaungu, Songambele Azimio na Msanda Muungano Wilaya ya Sumbawanga Vijijini Mkoani Rukwa na Taasisi ya Kidini ya Efatha ambayo ni mwekezaji katika Shamba la Malonje, Novemba 2023;

iii. Uchunguzi kuhusu tuhuma za Askari Polisi kumpiga, kumtesa na kumsababishia ulemavu mwananchi wa Manispaa ya Morogoro; Septemba, 2023;

iv. Uchunguzi kuhusu malalamiko dhidi ya Bi. Pauline Philipo Gekul na wenzake kudaiwa kuwafanyia vitendo vya ukatili na udhalilishaji Bw. Hashim Ally Philemon na Bw. Michael Isaria Marishamu, Desemba 2023;

v. Uchunguzi kuhusu tuhuma dhidi ya Askari wa Jeshi la Polisi Kituo cha Polisi Kati Dodoma kumkamata mkazi mmoja wa Mtaa wa National Housing, Kata ya Makole, kinyume na utaratibu wa kisheria; Januari 2024. Uchunguzi huu ulianzishwa na THBUB kufuatia vyombo vya Habari kumnukuu na kumuonesha mkazi wa Mtaa wa National Housing, Kata ya Makole akiwalalamikia askari Polisi kwa kumkamata kinyume na utaratibu wa kisheria na kumtesa wakati anahojiwa huku akiwa amevuliwa nguo katika Kituo cha Polisi kwa tuhuma za kuvunja duka;

vi. Uchunguzi kuhusu tuhuma dhidi ya Askari wa Jeshi la Polisi, Mkoani Kilimanjaro kumnyanyasa, kumdhalilisha, kumuweka mahabusu na kumfungulia kesi isivyo halali, mkazi wa Moshi, Kilimanjaro, Machi, 2024;

vii. Uchunguzi kuhusu tuhuma dhidi ya Askari wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Mbarali kumtesa na kumfanyia vitendo vya ukatili mfanyabiashara na mkazi wa Ubaruku, wilaya ya Mbarali; Aprili, 2024;

viii. Uchunguzi kuhusu Baa ya CASK (CASK Bar and Grill) iliyoko Kata ya Nyamanoro, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Jijini Mwanza, kuharibu mazingira kwa kelele na kutotekeleza amri zilizotolewa na mamlaka halali za kusitisha kelele; Aprili 2024;

ix. Uchunguzi kuhusu malalamiko dhidi ya mgodi wa North Mara kudaiwa kutozingatia utaratibu wa utwaaji wa ardhi mwaka 2021 na 2022, kwa kuwaondoa kwa nguvu wananchi wa vijiji vya Komarera na Kewanja katika ardhi yao, matumizi ya nguvu, vitisho, ukatili na udhalilishaji wakati wa zoezi la kupanua eneo la uchimbaji madini; (Aprili 2024).

x. Tuhuma dhidi ya Askari wa Hifadhi ya Taifa ya Rubondo Mkoani Geita kufanya vitendo vya ukatili na mateso kwa Wananchi wanaoingia ndani ya Hifadhi, Mei 2024;

xi. Uchunguzi kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kutwaa ardhi ya Kijiji cha Ludewa, wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe bila kufuata utaratibu, Mei, 2024. Katika lalamiko hilo, Wananchi walidai kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilichukua eneo la hekari 125 kinyume na makubaliano na utaratibu na kulipatia hati miliki eneo hilo kwa Shule ya Sekondari Isandula mwaka 2012 ambapo Wananchi hao walidai kuwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, pamoja na hatua alizochukua kuyapatia ufumbuzi malalamiko hayo lakini suluhu haikupatikana.

xii. Uchunguzi wa lalamiko kuhusu tukio la mkazi wa Kijiji cha Mchomolo, Kata ya Mchomolo, Tarafa ya Undendeule, Wilaya ya Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma kuchomwa moto mikono na kumsababishia ulemavu wa kudumu; Mei 2024;

xiii. Uchunguzi kuhusu uchafuzi wa mazingira unaotokana na maghala ya TAZARA kutiririsha sumu (tindikali aina ya Sulphur) kwenye makazi ya wananchi, Mei 2024. Uchunguzi ulitokana na THBUB kupokea malalamiko kutoka kwa mkazi wa mtaa wa Mwale, Kata ya Mnazi Mirefu, Wilaya ya Ilala Mkoa wa Dar es Salaam akilalamikia Shirika la Reli TAZARA kujenga maghala yanayohifadhi kemikali ya Sulphur karibu na makazi ya watu na kusababisha madhara kwa wakazi wanaoishi jirani na maghala hayo, kama vile kupumua kwa shida, vikohozi na kutokwa na upele sehemu mbalimbali za miili yao. Ingawa wamewasilisha madai yao sehemu mbalimbali hakuna hatua zilizochukuliwa.

xiv. Uchunguzi kuhusu tuhuma dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha kutoa amri ya kukamatwa na kuwekwa mahabusu mkazi wa Mkoa wa Arusha kinyume na utaratibu wa kisheria, Juni, 2024.

## 3.0 MATOKEO YA CHUNGUZI HIZO

**Ndugu Wanahabari;**

Katika baadhi ya chunguzi, THBUB ilipata ushahidi na vielelezo vilivyothibitisha vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Yafuatayo ni maelezo ya matokeo ya chunguzi katika maeneo ya ardhi, uharibifu wa mazingira, hifadhi za Wanyamapori;

vitendo vya kikatili na vipigo kwa wananchi na matumizi mabaya ya madaraka kama inavyoainishwa hapa chini.

### 3.1 Chunguzi zilizohusu migogoro ya Ardhi

**Ndugu Wanahabari;**

Katika baadhi ya chunguzi zilizofanyika kuhusiana na masuala ya ardhi THBUB imebaini baadhi ya migogoro kuwa ya muda mrefu na kusababisha matukio ya uvunjifu wa amani, lakini pia walalamikaji/wananchi kutokuwa wamiliki halali wa maeneo ambayo ni chanzo cha mgogoro.

Uchunguzi wa mgogoro wa ardhi katika shamba la Malonje Wilaya ya Sumbawanga Mkoani Rukwa dhidi ya Taasisi ya Kidini ya Efatha, THBUB ilibaini kuwa Taasisi ya Kidini ya Efatha ni mmiliki halali wa Shamba la Malonje na tangu amekabidhiwa shamba hilo mwaka 2008 kumekuwa na mgogoro wa mipaka kati yake na wananchi. Migogoro hiyo imesababisha matumizi ya silaha za moto na kujeruhi wananchi hususan katika tukio la tarehe 6 Novemba, 2024 ambapo wananchi watatu walipigwa risasi.

Katika uchunguzi dhidi ya uongozi wa Kijiji cha Mbabala B kutwaa ekari 37 za Wananchi,THBUB ilijiridhisha kuwa utaratibu wa kisheria wa utwaaji wa ekari 37 haukuzingatiwa.

Vilevile, katika uchunguzi kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kutwaa ardhi ya Kijiji cha Ludewa, wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe bila kufuata utaratibu, THBUB imebaini kuwa eneo la ekari 125 ambalo ni chanzo cha mgogoro lilimilikishwa kwa shule ya Sekondari Isandula kihalali na hivyo madai ya Wananchi hayakuthibitishwa. Aidha THBUB ilibaini kutokuwepo kwa uwazi na ushirikishwaji katika utoaji wa taarifa za mgogoro husika kwa

Wananchi na hasa walalamikaji ili kuwa na uelewa wa pamoja kuzuia vitisho vya matumizi ya nguvu na uvunjifu wa amani dhidi ya jumuiya shule husika kutokana na mgogoro huo.

Aidha, katika Uchunguzi kuhusu malalamiko ya wananchi wa vijiji vya Komarera na Kewanja dhidi ya mgodi wa North Mara, THBUB imebaini kwamba, Mgodi wa North Mara ulitwaa ardhi yenye ukubwa wa Ekari 652 katika Kijiji cha Komarera kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za mgodi na zoezi la uthamini na utwaaji wa eneo husika lilifuata taratibu na lilifanyika kwa uwazi na ushirikishwaji wa pande zote na wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa walilipwa fidia stahiki. Aidha, THBUB imebaini kuwepo kwa matukio ya vifo na madhara mbalimbali yanayotokana na mapambano baina ya vijana wanaoishi karibu na mgodi ambao huvamia mgodi na Askari wa Jeshi la Polisi wanaolinda Mgodi wa North.

**3.2 Uchunguzi wa tuhuma za uvunjifu wa haki za binadamu katika maeneo ya Hifadhi**

**Ndugu Wanahabari;**

Katika uchunguzi wa tuhuma dhidi ya Askari wa Hifadhi ya Taifa ya Rubondo Mkoani Geita kufanya vitendo vya ukatili, mateso na matumizi ya nguvu kupita kiasi kwa Wananchi  wanaoingia ndani ya Hifadhi, THBUB ilibaini kuwepo kwa vitendo vya ukatili na mateso vilivyosababishwa na Askari wa Hifadhi. THBUB imebaini pia kuwa mahusiano baina ya Watendaji wa Hifadhi na Wananchi siyo mazuri.

### 3.3 Chunguzi kuhusu uharibifu wa mazingira

**Ndugu Wanahabari;**

Katika chunguzi zilizohusu uharibifu wa mazingira, THBUB ilithibitisha kuwa Baa ya CASK ilifanya uharibifu wa mazingira kwa kwa kusababisha kelele zilizopita viwango kwa mujibu wa sheria, hivyo kuwasumbua wakaazi wa jirani na ilipo baa hiyo na pia Baa hiyo ilikiuka masharti ya leseni ya ukumbi wa starehe kwa kuendesha biashara hadi alfajiri (kukesha). Aidha Bar hiyo, ilikiuka amri halali zilizotolewa na Baraza la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), kwa kukataa kusitisha kupiga kelele za muziki na kukataa kulipa faini za Shilingi 2,000,000/= na 5,000,000/- walizotozwa kwa vipindi tofauti.

Katika uchunguzi kuhusu Maghala ya TAZARA, THBUB imebaini ukiukwaji wa miongozo ya usimamizi wa Maghala yanayohifadhi kemikali ya sulphur, yaani "guidelines for management of bulk Sulphur", vile vile taratibu za kuzingatiwa kabla ya kuanza kuhifadhi kemikali hizo hali ambayo ilisababisha kutokea milipuko mitatu ya kemikali ya sulphur katika eneo husika ikiambatana na vumbi, sulphur kuvuja barabarani jambo linalohatarisha maisha ya binadamu.

### 3.4 Chunguzi za tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi

**Ndugu Wanahabari;**

Baadhi ya chunguzi zilizofanyika dhidi ya Jeshi la Polisi, THBUB ilithibitisha kutozingatiwa kwa taratibu za kisheria za ukamataji na ushikiliwaji wa watuhumiwa katika mahabusu za Jeshi la Polisi. Vitendo hivyo viliambatana na wananchi kupigwa, kufanyiwa ukatili na mateso na

kuwasababishia majeraha. Mfano; katika lalamiko la mwananchi kutoka Manispaa ya Morogoro, THBUB ilijiridhisha kuwa mwananchi huyo alipigwa na kufanyiwa vitendo vya kikatili vilivyomsababishia majeraha akiwa anashikiliwa na Askari wa Jeshi la Polisi, Mkoani Morogoro.

Kadhalika katika lalamiko la tuhuma dhidi ya Askari wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Mbarali kumtesa na kumfanyia vitendo vya ukatili mfanyabiashara, ushahidi ulithibitisha kuwa mfanyabiashara huyo aliwekwa mahabusu bila kupewa dhamana kwa zaidi ya siku ishirini, kufanyiwa vitendo vya kikatili vilivyosababisha majeraha mikononi kutokana na kufungwa pingu wakati akiteswa pia alipatikana na kidonda kikubwa sehemu ya unyayo wa mguu wa upande wa kulia kutokana na kupigwa. Pamoja na madhila hayo Mwananchi huyo hakupatiwa matibabu kwa wakati.

Katika uchunguzi kuhusu tuhuma dhidi ya Askari wa Jeshi la Polisi katika Kituo cha Polisi Kati Dodoma, THBUB ilithibitisha pia kutozingatiwa taratibu za kisheria wakati wa ukamataji na kumshikilia mtuhumiwa ikiwa ni pamoja na kutopatiwa dhamana, kufanyiwa vitendo vya kikatili kwa kupigwa na kuteswa. Aidha THBUB ilibaini baadhi ya vituo vya Polisi vinatumika mahsusi kwa ajili ya kuwatesa watuhumiwa wakati wa mahojiano kabla ya kuwafikisha katika vituo vingine vya Polisi.

Hata hivyo, katika uchunguzi wa tuhuma zilizotolewa na mkazi wa Moshi dhidi ya Askari wa Jeshi la Polisi, Mkoani Kilimanjaro kumdhalilisha na kumfungulia kesi bila kuzingatia utaratibu wa kisheria, hazikuthibitika.

## 3.5 Chunguzi zilizohusu matumizi mabaya ya madaraka

**Ndugu Wanahabari;**

Kuhusu chunguzi zilizohusu matumizi mabaya ya madaraka, THBUB ilibaini mwenendo usiozingatia maadili kwa baadhi ya viongozi wa umma.

**Ndugu wanahabari;**

Katika tukio mojawapo ya matukio, Mheshimiwa Pauline Gekul alihusishwa na tukio la kuwaingiza chupa sehemu ya haja kubwa Bw. Hashim Ally na Bw. Michael Isaria. Baada ya uchunguzi THBUB kwa kuzingatia maelezo ya watu mbalimbali waliohojiwa na vielelezo ambavyo THBUB ilivipitia haikubaini suala hilo kufanyika. Hata hivyo, THBUB ilibaini kuwa walalamikaji walizuiliwa kwa muda mrefu wakati wakihojiwa na mlalamikiwa kuhusu tuhuma za kutaka kumwekea sumu Bi. Pauline Gekul pamoja na kupeleka madawa ya kishirikina katika hoteli yake iitwayo Paleii Lake View na hivyo kusababisha walalamikaji kukosa haki yao ya kuwa huru.

Malalamiko mengine yalikuwa dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Paul Makonda. Katika uchunguzi dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha kutoa amri ya kukamatwa na kuwekwa ndani ya mahabusu ya Polisi mkazi mmoja wa Arusha, THBUB baada ya uchunguzi imebaini kuwa amri iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa haikuwa halali na haikuzingatia aina ya makosa na utaratibu ulioainishwa kisheria wa utekelezaji wa mamlaka hayo na kwamba mwananchi huyo hakuwa mhusika wa madai ya msingi ambayo Mkuu wa Mkoa huyo aliyatumia kushughulikia suala lililokuwa mbele yake. Ilibainika pia kuwa Mkuu wa Mkoa huyo alivuka mipaka ya majukumu yake kwa kushughulikia na kutoa maamuzi katika suala ambalo lilipaswa kufuata mkondo wa kisheria wa kimahakama kwa kuwa madai hayo yangeshughulikiwa kama shauri la daawa. Aidha, hata kama kulikuwa na viashiria vya makosa ya kijinai, njia sahihi ingekuwa ni kulielekeza Jeshi

la Polisi kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. THBUB pia ilibaini kutozingatiwa kwa haki za mtuhumiwa kwa kuwekwa mahabusu kwa saa 96 yaani siku 4 bila ya kufunguliwa mashtaka. Pamoja na kuitwa kutoa maelezo mbele ya THBUB ili kuwasilisha utetezi wake Mkuu huyo wa Mkoa alikaidi kufika mbele ya THBUB.

## 4.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA YA THBUB KUTOKANA NA CHUNGUZI ZILIZOFANYIKA

**Ndugu Wanahabari;**

Taarifa za chunguzi zenye mapendekezo kwa kila uchunguzi uliofanyika zimekwisha wasilishwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji na baadhi zinakamilishwa. Mapendekezo ya jumla yaliyotolewa katika taarifa hizo ni kama ifuatavyo:

i. THBUB imependekeza kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha Askari wanapata mafunzo ya mara kwa mara ya kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ikiwemo mafunzo ya haki za binadamu na utawala bora ili kuwajengea weledi katika kutekeleza majukumu yao;

ii. Mkuu wa Jeshi la Polisi kuweka CCTV Camera katika vituo vya Polisi, hususan kwenye kaunta (CRO) zote za Vituo vya Polisi ili kubaini matukio yote yanayoendelea kwa mahabusu na raia wanaofika katika vituo hivyo kwa sababu mbalimbali;

iii. Mkuu wa Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua za kinidhamu Maafisa na Askari wa Jeshi la Polisi waliohusika katika vitendo ya kuwapiga na kuwatesa watuhumiwa kama ilivyobainishwa;

iv. Katika eneo la Hifadhi, mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Maliasili zishirikiane na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzipitia sheria zinazohusiana na Hifadhi ili kuondoa kasoro zilizopo katika Sheria za Hifadhi, kuchukua hatua dhidi ya Askari wa Hifadhi ambao wanatuhumiwa kufanya vitendo vya ukatili na mateso dhidi ya Wananchi. Aidha, Mamlaka za Serikali ziimarishe mahusiano baina ya Wananchi na Mamlaka ya Hifadhi ikiwa ni pamoja na kutafuta njia mbadala kuwezesha Wananchi kiuchumi ili kupunguza vitendo vya ujangili;

v. Wizara ya Madini washirikiane na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Uongozi wa Mgodi wa North Mara ili kutenga maeneo ya uchimbaji madini kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo kuondoa uvamizi kwenye Mgodi wa North Mara;

vi. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na wadau wa ulinzi na usalama nchini kuandaa Mpango mkakati wa pamoja wa kuimarisha ulinzi katika miradi mikubwa ya kimkakati ya kitaifa ikiwemo miradi katika sekta ya uziduaji.

vii. Mamlaka mbalimbali za Serikali, Mwekezaji Taasisi ya Kidini ya Efatha pamoja na wananchi kukubaliana kutatua mgogoro wa Shamba la Malonje kwa kupima eneo la ardhi linalobishaniwa la Taasisi ya Kidini ya Efatha hasa katika Kijiji cha Sikaungu, na kushauriana na mwekezaji kuwaachia Wananchi hao eneo hilo kuendelea na shughuli za kilimo na ufugaji kama njia ya kuleta amani na maelewano huu ni ushauri wa THBUB;

viii. Viongozi wa Umma wanapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi wakati wote anapotekeleza majukumu yao na siyo kujichukulia sheria mkononi;

**MWISHO**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kufanya Chunguzi katika matukio yanayojitokeza na yenye viashiria vya uvunjifu wa amani nchini, ili kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa mara moja katika jamii.

**Na Kazi Iendelee!**